**LBE Komputa na Intaneti - Programme 7**

Mwandishi : Richard Lough

Muharii: Maja Dreyer

Tafsiri : Eric Ponda

**Wahusika:** Beatrice (Msichana wa Makamu), John (Mvulana wa Makamu), Komputa (Sauti), Mtaalam ( Sauti ya Mwanmume kutoka Studio)

**Clips (English) to be overvoiced:** Daudi Were (Mvulana wa Makamu), Benson (Miaka 25- Mtaalam wa ubunifu wa kurasa za mtandao)

Sauti za Watu wengine: Msimulizi kutoka Studio.

Music – [**Full up for 0:10 then fade under Intro]**

**Intro 7.1**

Hujambo na karibu kwa makala mengine ya Noa Bongo jenga maisha yako kuhusu masuala ya Komputa na Intaneti. Katika sehemu hii ya saba, Beatrice na John wanajifunza kuwa mtu anaweza kutumia mtandao wa Intaneti kusikiliza muziki na kutazama kanda za Video. Lakini je, huduma hizi ni za bure au ni za malipo? Na vipi unaweza kupata huduma hizi.? Unganasa nasi ujifunze mengi……

**SFX Komputa ikijifungua[Fade under…]**

**1. Komputa:** Hujambo John na Beatrice…

**2. John/Beatrice** Habari Komputa…

**Full Up SFX_Komputa ikijifungua**

**3. Komputa:** Hebu subirini kidogo nijiunganishe na mtandao wa Intaneti ….ahhh…..

**SFX_Mtandao umeunganishwa**

**4.Komputa:** Sawa Kabisa… sasa tumeunganishwa. Naweza kumsaidia vipi leo?

**5. Beatrice:** Jana nilikuwa nikisikiliza vipindi na muziki kupitia redio. Kisha mwisho wa kipindi, wanasema unaweza kukikisikiliza tena kipindi hicho kupitia mtandao wa Intaneti .Kadhalika wanasema unaweza kufungua muziki na kanda za Video kwenye mtandao huo. Inawezekana kweli? Nilidhani Intaneti ni maandishi pekee.?

**6. Komputa:** Ndio hilo linawezekana, ni rahisi kabisa. Lakini kuna mambo kadhaa ya kiteknolojia ambayo ni lazima ujifunze kwanza .

**7. John:** Sio tena mambo hayo ya teknolojia!.

**8. Komputa :** Ni rahisi, hilo nakuhakikishia John…! Kwanza kabisa ili kufungua ukurasa wako wa sauti kama vile Muziki, unahitadi mtandao wenye kasi zaidi kuliko ule unaotumia unapofungua kurasa wa maandishi..

**9. Beatrice:** Na pia unahitaji kasi tofauti unapofungua ukurasa wa Video?

**10. Komputa:** Ndio. Ili kuzikiza sauti kama muziki, unahitaji mtandao wenye kasi isiyopungua ***kilo bites 28.8,*** na pia ***Kilobites 56.6*** kwa kanda ya Video yenye kasi ya pole pole na ***100kbps*** kwa Video ya kasi. Kumbuka unaweza pia kumuuliza mwenye mkahawa wa huduma za Intaneti jinsi ya kufungua ukurasa wa kasi zaidi katika mtandao wako.

**11. Beatrice:** Je unaweza kupata mitandao yenye kasi hizi kwa urahisi?

**12. Komputa** Kurasa nyingi za tovuti ulimwenguni, hutoa huduma za hadi kasi ya ***Kilobites 300*** , Kwa hiyo si tatizo. Lakini vipimo hivi bado havijawasili katika mataifa mengi barani Africa.

**13. John:** Hivyo unamaana hatuwezi kusikiliza muziki au kutazama kanda za Video?

**14. Komputa:** Unaweza kutazama Video na pia kusikiza muziki lakini itakuchukua muda kufungua ukurasa wenyewe. Pia utahitadi kupata data maalum kutoka kwa mtandao wa Intaneti kama vile ***Real Player*** au ***Windows Media***. Hizi zitakusaidia kuzikiza Muziki na pia kutazama kanda za Video. Ni rahisi..sasa munaweza kuendelea.

**15. Beatrice:** Sawa kabisa ! John unaweza kukumbuka Muziki, au kanda tunazoweza kucheza kwa mtandao.

**[SFX Habari za DW_kupitia Mtandao]**

Ni sawa na Telvisheni tu lakini kupitia mtandao..

**SFX_Typing + SFX_Double_Mouse_Click**

**SFX_You_Tube_Video**

**16. Beatrice:** John, Nimefungua ukurasa mwengine unaofahamika kama ***You Tube***. Unakanda za Video kutoka kwa ile bendi maarufu tulisikia ikicheza jana usiku, hebu njoo uone!.

**17. John:** Ni maajabu haya, ni kama Mtu anayetazama Televisheni. Na hebu angalia hii nyingine.

**18. Komputa:** Na vile vile pia unaweza kuweka kanda yako ya Video kwenye mtandao huu. Huo ndio uzuri wa mtandao wa Intaneti. Ni mtandao unaokuwezesha kutangamana, kila Mmoja wetu anaweza kushirikishwa. Kadhalika unaweza kufungua ukurasa wa ***myspace dot com***.

**19. Beatrice:** Baadaye naenda kukutana na Daudi, mtalaam wa masuala haya ya mtandao nchini Kenya. Yeye. ana programu na vifaa vya aina mbali mbali za kurekodi na kucheza muziki na kanda za video katika mtandao wake.

**20. Komputa**: Zinafahamika kama ***podcasting***. **[SFX_DW_Podcast]** Huu ni utalamu wa kutumia Microfoni kurekodi sauti kwenye komputa..

**21. John**: Siku hizi zinatumika kila mahali?

**22. Komputa**: Ndio ! Kwanza mitandao mingi ya kibiashara na vituo vya habari vinavyopeperusha matangazo kupitia mtandao, hutumia vifaa hivi au teknolojia hii ya Podcast au Video. Mfumo huu ndio unaofahamika kama multi media na ni mfumo ambao huenda ukategemewa zaidi siku za usoni..

**23. John:** Sijui kama kina mtandao mzuri Africa tunaoweza kutembelea Beatrice.

**SFX_Akiandika kwenye Komputa**

**24. Komputa :** ***Pambazuka dot org*** ni mzuri, munaweza kuanza nao.. Huwa wanaangazia masuala yote, na pamoja na hayo Mtu anaweza kufungua ukurasa wa ***Podcast*** au Video. Kwa habari kuhusu bara la Africa na masuala mengineyo, huu ndio mtandao unaoweza kuutumia kwa sasa..

**25. John:** Pia nimesikia mtandao wa habari za Africa unaojulikana ***www dot all Africa dot com.***

**SFX_Double_Mouse_Click**

**26. Beatrice:** Sasa najaribu kufungua mtandao huu wa ***all Africa dot com.***

**27. John:** Hebu tazama, pia unaweza kusoma, kuangalia na pia kusikiza habari zote zikiwemo za michezo.

**SFX_Muziki [wowote]**

**28. Komputa:** Sasa nimejua jinsi ya kufungua ukurasa wa kucheza muziki na kanda za Video. Nadhani itakuwa vigumu sisi kutengana.

**29. Beatrice:** Asante sana Komputa!

**Muziki (fade under…)**

**SFX_Ambie_AccessKenya**

**1. Beatrice:** Habari Daudi. Nimekuwa nikisoma kuhusu ukurasa wa ***blog*** yako ***mentalacrobatics dot com***. Sijawahi kukutana na Mwafrica mtaalam wa ubunifu wa kurasa za ***Bloggy*** . Ni jambo zuri kuwa mtaalam wa aina hii?

**Clip: 7.2_Were_1**

Ehh ni jambo zuri kuwa Mtaalam wa ***Bloggy***. Ni moja wapo na mambo ya Kiafrica unayoweza kufanya katika mtandao. Hii yote ni kujaribu kutangamana na watu wa maeneo mbali mbali , kujenga jamii ya Kiafrica. Lakini pia inahitaji teknolojia ya hali ya juu ambayo mimi naitaka.

**2. Beatrice:** Lakini ***ku- Blog*** ni kufanya nini hasa? Na kuna haja gani ya kubuni ukurasa wa ***Blog*** kama kunakurasa nyingi tu kwenye mtandao?

**Clip: 7.2_Were_2**

Ukurasa huu wa ***blog,*** ni ukurasa wa mtandao ambao unaweza kuurekebisha wakati wowote kulingana na mabadiliko. Uzuri wa ukurasa huu huweka kando masuala yote ya teknolojia na kuzingatia tu yale unayotaka kufanya.

**3. Beatrice** Kwa hivyo unaweza kufungua ukurasa huu wa ***blog*** moja kwa moja?

**Clip: 7.2_Were_3**

Kabisa,! ni miongoni mwa mambo rahisi mtu anaweza kufanya katika ulimwengu huu wa teknolojia na utanda wazi.

Kuna kurasa nyingi bila malipo ambazo zinatoa huduma za kubuni ***Blog.*** Ni rahisi tu kama kufungua akaunti ya ***e-mail*** katika ukurasa wa ***yahoo, gmail au hotmail***.

**4. Beatrice:** Sasa nitaandika nini katika ***Blog*** hii? Inaonekana unafahamu vyema siasa za Kenya. Je ni lazima niwa najua mambo yote haya ndipo niandika ***Blog?***

**Clip: 7.2_Were_4**

Cha msingi kwanza ni kujua unataka kuandika kuhusu nini, ambacho watu wengine ulimwenguni unataka

wajue. Kila mmoja wetu ana kitu anachokipenda au anachoweza kukipenda maishani.

**5. Beatrice**: Asante Daudi, ni matumaini yangu kwamba nitaweza kufuatilia yote yaliko kwenye ***Blog*** yako ya ***mentalacrobatics dot com blog.***

**SFX__ Mazingira ya Ofisi.**

**6. John:** Nimekuja kukutana na Besnon mwenye umri wa miaka 25 ofisini mwake. Benson kuna kurasa nyingi tu katika mtandao wa Intaneti na nilitaka unieleze jinsi ninavyoweza kufungua ukurasa wangu wenyewe.

**Clip: 7.2_Benson_1**

Si vigumu kufungua ukurasa, cha msingi unachohitaji ni ukurasa unaoweza kuandikia na kuchora grafu.

**7. John:** Na je utawezaje kubuni ukurasa ambao si rahisi kuvamiwa?

**Clip: 7.2_Benson_2**

Iwapo unataka kujumuisha mambo mengine kama vile ***Blogs***,kurasa za mawasiliano ya moja kwa moja na injini za uchunguzi yaani ***Search Engines***, unahitaji kupata mafunzo kuhusu programu za Intaneti..

8. **John:** Kama gani?

**Clip: 7.2 Benson_3**

Kwa mfano ukurasa wa kawaida unahitaji kujua kuhusu ***html,*** lakini iwapo unataka ukurasa huo uwe wa hali ya juu, basi lazima ujifunze lugha za programu nyingine zitakazokuwezesha kuelewa mambo haya kwa urahisi.

**SFX: Beep sound (should always be used to introduce the expert, like somebody answering in a quiz show)**

**9. Mtaalam :** Samahani kwa kukukatiza,John, huyu ni mtaalam wako kutoka Studio. ***HTML*** inamaanisha ***hyper text markup,*** hii ni lugha ya kiteknolojia inayoweza tu kusomwa na Komputa kama vile sisi tunavyoweza kusoma Kingereza au Kifaransa.

**19. John:** Ahha, hii ni ngumu zaidi kuelewa kuliko hata teknolojia ya ***Ku-Blog***. Nadhani ni lazima uwe unaelewa mambo ya Komputa Benson?

**Clip: 8.2_Benson_5**

Ukiwa mbunifu wa kurasa za tovuti kwenye Intaneti, kwanza ni lazima ujifunze mambo haya . Mambo yanaenda yakibadilika. Miaka miwili iliyopita watu walikuwa wakitumia lugha tofauti na ile inayotumika hivi sasa.

**11. John:** Je nikitaka kutumia komputa nikiwa Mzee, nifanyeje

**Clip: 8.2_Benson_6**

Katika Teknolojia ya mawasiliano, kuna mambo mengi sana Mtu anaweza kufanya, si lazima ume mbunifu wa kurasa za tovuti, unaweza kuwa mtaalam wa masuala ya ***Data*** za Komputa, unaweza kuwa mbunifu wa aina za ***Software*** au ***Hardware*** kushughulikia matatizo yote yanapotokea kwenye mtandao wa Intaneti au Komputa.

**12. John** Ni kana kwamba ulimwengu umejaa mengi ya kujifunza hasa katika teknolojia ya kupitia Komputa na mtandao wa Intaneti!

**Outro**

Na ni hayo tu tuliyoweza kukuletea katika kipindi cha leo. Kumbuka leo tumejifunza kwamba ni rahisi na unaweza kubuni blogi bila malipo, na ni njia bora zaidi ya kubadilishana mawazo na ulimwengu. Iwapo unataka kukisikiliza tena kipindi hiki, unaweza kutembelea tovuti yetu kwenye mtandao: www.dw-world.de/lbe Hadi wakati mwengine kwaheri.

**Mwisho**